

ITILIMA IMEPOKEA SHILINGI BILIONI TANO KATIKA SEKTA YA ELIMU PEKEE: OLE NASHA

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. William Ole Nasha amezindua Mradi wa Mabweni maalum ya Wanafunzi wa Kike katika shule ya Sekondari Nkoma wilayani Itilima, yaliyo jengwa kwa ufadhili wa Ubalozi wa Jamhuri ya Watu wa China kwa kushirikiana na Halmashauri ya Itilima na Wananchi wa Kata ya Nkoma.

Akiwa wilayani humo Mhe. Olenasha aliupongeza uongozi wa Halmashauri ya (W) Itilima na Wananchi wa Kata ya Nkoma kwa kusimamia na Kushiriki katika ujenzi huo kwa hali na mali kwa lengo la kuhakikisha wanapunguza changamoto zinazo wakabili watoto wa Kike kushindwa kutimiza malengo yao ya kupata elimu na kujikomboa kimaisha.

Aidha Mhe. Ole Nasha aliwataka wanafunzi wa shule hiyo kuhakikisha wanasoma kwa bidii na kuamini kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli anawapenda sana na ndiyo maana mpaka sasa Serikali yake imeshatumia kiasi cha tsh. bilioni 945/ katika sekta ya elimu na Wilaya ya Itilima pekee, imepata tsh. bilioni tano.

“Rais alipo niteuwa kuwa Naibu Waziri wa Elimu aliniambia nenda kaongee na Wanafunzi, Walimu na Viongozi wao ilikujuwa changamoto zinazo wakabili na katika hili ndiyo maana Mhe. Rais Magufuli ameelekeza pesa nyingi sana katika elimu na kutatua changamoto hizo” alisema Mhe. Olenasha.

Akijibu baadhi changamoto zinazo ikabili shule ya Sekondari Nkoma zilizo elekezwa kwake na Mbunge wa jimbo la Itilima Mhe. Njalu Daudi Silanga ambazo ni kutokamiliwa kwa Maabara na ukosefu wa Nyumba za Walimu Mhe. Naibu Waziri alisema;

” Nawaahidi naenda Wizarani kutafuta pesa za ukamilishaji wa Maabara hii na nitawajengea nyumba ya Walimu itakayo kaliwa na familia nne”

Vilevile Mhe. Ole Nasha alikagua Mradi wa ujenzi wa jengo la Mthibiti Ubora wa Elimu ambalo limegharimu kiasi cha tsh. Milioni 157 na Mradi wa ujenzi wa majengo ya Chuo Cha Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) ambacho kinajengwa katika kata ya Chinamili wilayani Itilima.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Technolojia aliweza kuongea na Wanafunzi wa Kata ya Nkoma, Lagangabilili na Chinamili na kuwashamasisha kutumia fursa iliypopo kujipatia elimu na kufanya Jitihada kupata matokeo mazuri.

Ujenzi wa mradi wa Mabweni mawili katika shule ya Sekondari Nkoma uliyo gharimu kiasi cha Tsh. milioni 304.7 ambapo Ubalozi wa China ulitoa kiasi cha Tsh. Milioni 178.4, Halmashauri ya Itilima Tsh. Milioni 99.5 na Mchangwa Wananchi Tsh. Milioni 26.7 umekuja baada ya kubaini changamoto za ufauru hafifu, mimba na Utoro zinazo wakabili wanafunzi hususani Watoto wa kike wa Kata ya Nkoma yenye Vijiji saba viliyopo umbali mrefu kutoka shulen hapo.